

**MOST na utafiti unaogharamiwa na mradi B@bel:  
Lugha kwenye Mtandao**

Sue Wright  
Chuo Kikuu Cha Aston  
[s.m.wright@aston.ac.uk](mailto:s.m.wright@aston.ac.uk)

**Chanzo cha utafiti**

Utafiti huu ulitayarishwa kufuatana na mradi wa UNESCO Initiative B@abel na unaowakusanya wanataaluma wa aina mbalimbali. Mradi huu ulibuniwa kukuza tamaduni za aina mbalimbali kwa ujumla na hasa kutafuta njia za kulinda lugha ambazo hazitumiwi sana duniani. Timu ya watafiti<sup>1</sup> iliombwa kutafuta njia za kukusanya data juu ya matumizi ya lugha kwenye Mtandao ili kupanga sera katika eneo hilo kufanyike kukiwa taarifa sahihi.

Kulikuwepo maswali-njia ya utafiti kadhaa, yakiwemo :

- Je, lugha ambazo zinaweza zikafifia na zile ambazo hazitumiwi sana zinaweza kukuzwa kati ya wazungumzaji wake zikiachiwa nafasi ya matumizi kwenye Mtandao?
- Je kuna aina mpya za lugha zinazotokana na kutumia njia ya maandishi katika kuwasiliana, njia ambayo inachukua aina nyingi za lugha ya kuzungumza ?
- Je, Mtandao unachangia katika kukutana kokote kule kwa lugha ?

Kuna wazo linalozagaa kuwa Kiingereza ni lugha ‘tawala’ kwenye Mtandao na kuwa kuwepokwake kunakataza matumizi ya lugha nyingine. Utafiti huu unaeleza na kutoa swali juu ya baadhi ya maelezo ambayo ni msingi wa jambo hilo na kubainisha hoja za kuunga mkono au kukana wazo hilo. Utafiti ulizingatia maeneo mawili

- jinsi gani Kiingereza ni chombo cha mitiririko ya habari kwenye mtandao ambazo hazijawahi kupatikana
- jinsi gani Kiingereza ni lugha iliyochaguliwa kwa mawasiliano kwenye Mtandao na makundi na mitandao.

Utafiti huu unaelezwa kwa undani zaidi kwenye gazeti pepe MOST na ripoti hii ni ufupisho wa baadhi ya matokeo yake.

**Namna ya kufanya utafiti**

Utafiti wa siku hizi juu ya nani anayetumia nini kwenye Mtandao unatokana kwa upana na hesabu za matokeo kwenye tovuti. Tuliwaza kuwa metodolojia hii haingekubaliwa, hasa kwa sababu kutazama tovuti haimanishi lazima kuwa habari hiyo imesomwa. Kuzuru tovuti kunaweza kuachwa mara tu inapoonekana kwa msomaji kuwa ni lugha ambayo haijui. Mkakati mwingine na wa maana zaidi ungekuwa kuwahoji watumiaji juu ya lugha ambazo

---

<sup>1</sup> Watafiti wa mwanzo mwanzo walikuwa David Block (Chuo cha Elimu, London), helen Kelly Holmes (Chuo Kikuu cha Limerick) na Sue Wright (Chuo Kikuu cha Aston).

wanazitumia kwenye Mtandao. Bila shaka, uhalali wa utafiti kama huo ungetegemea kupata sampuli ambayo ingewezekana kuitumia bila matatizo kujumuisha. Kundi lililochaguliwa ni la wanafunzi wa Chuo Kikuu. Tunawaza kuwa wanafunzi wa Chuo Kikuu ni labda kati ya wale wanaozoea kompyuta kuliko wengine katika jamii, wale ambao wana fursa ya kutumia kompyuta vyuoni na ambao wangekuwa na kiwango cha kisomi ambapo wanatakiwa kufanya utafiti bila kutegemea watu wengine. Kwa hiyo wanaweza kuwa na ujuzi, fursa na haja ya kutumia Mtandao.

Waliohojiwa walichaguliwa kutoka taaluma mbalimbali, lakini wote walikuwa wakisoma masomo ya Kiingereza, na ni kwa kupitia walimu wao wa lugha ya Kiingereza tulipowasiliana nao. Mantiki ya uamuzi ilikuwa kupata sampuli ambamo kila mhojiwa angejua si chini ya lugha mbili na lugha mbili, akimudu vizuri lugha ya kitaifa ya kufundishia na akiwa viwango mbalimbali katika Kiingereza. Kwa vile wote walikuwa wakisoma Kiingereza, kimsingi, wanategemewa kuwa wamewahi kutumia lugha hiyo kama chombo kwenye Mtandao kama wangetaka. Kwa hiyo tulikuwa na sampuli ambako kulikuwa orodha ya lugha ambazo wangeweza kutumia kwenye Mtandao na zile ambazo zinahitajika kweli kwenye Mtandao.

Hata hivyo, kwa sababu wanafunzi wa Chuo Kikuu wanaonekana, kwa mujibu wa wazo kuwa jamii huongozwa na wataalamu na weledi, kama kundi la wale ambao ni vigogo wa siku zijazo katika jamii zao, data juu ya matumizi yao ya lugha zinaweza kuonyesha itakavyokuwa katika wahusika wa kitaifa na kimataifa katika siku zijazo.

Kutokana na mialiko kwa idadi kubwa ya vyo katika mabara yote, data mwishowe zilikusanywa katika Vyu Vikuu na shule za sekondari za juu nchini Tanzania, Indonesia, Umoja wa Falme za kiarabu, Oman, Ufaransa, Italia, Poland, Macedonia, Ujapani na Ukraine. Nchi hizo kumi ni kama ziliwakilisha idadi ya hali za kilugha tofauti. Katika baadhi ya nchi, lugha ambayo inatumiwa tangu zamani inaonekana kweli kama yenye hadhi na mara kwa mara inasomwa kama lugha ngeni. Katika nchi nyingine, lugha rasmi ni vile vile lugha mahiri kwa nchi nyingi za eneo hilo na ambayo inasaidia mitandao ya hapo kufanya kazi. Katika baadhi ya makundi, kupata uhuru kulimaanisha kuwa lugha ya taifa bado inaendelea kutekelezwa ili itumiwe katika dhima na sehemu zote za maisha rasmi hadharani. Katika nchi zote kumi kulikuwa pia nchi ambazo zilikuwa na lugha tofauti chache na nyingine ambazo lugha zilikuwa na lugha tofauti nyingi sana. Kwa hiyo, ingawa kuna sehemu kadhaa duniani ambapo hatukuweza kupata usalama wa washiriki, tunawaza kuwa tulivyowasambaza kuliwakilishwa hali nyingi za lugha zilivyo.


Kifaa tulichotayarisha kutathmini uchaguzi na matumizi ya lugha kilikuwa hojaji ambayo iliomba wanafunzi kutoa majibu kamili juu ya matumizi yao ya lugha na kuonyesha lugha na lengo la mfululizo wa vipindi kumi vinavyofuatana. Tulihisi kuwa, ingawa hojaji ilizingatia maswali ya watu kuhusu matumizi yao, kuwaomba majibu kamili kulikuwa na maana ya kujaribu kuwa na makosa machache katika kueleza namna wanaotumia lugha. Wahojiwa wangehitaji kufanya wawezavyo kuyaunda.

## **Matokeo**

Pamoja na majibu zaidi ya 3000 kwa hojaji, tunawaza kuwa tulipata ujuzi wa matumizi yanavyoendelea katika matabaka ya wasomi pote duniani.

Tokeo la kwanza lilikuwa kwamba makundi yanayofanana sana katika Vyu Vikuu tofauti yalitoa tathmini tofauti sana ya ustadi wao wa lugha ya Kiingereza. Wahojiwa Wamacedonia 92% walidai wote kuwa wana viwango vya ujuzi ambavyo vingewawezesha kutumia lugha

hiyo bila matatizo kutumia Mtandao. 77% za sampuli ya Waukraine 55% wanawaza kuwa wana kiwango cha ustadi wa Kiingereza unaofaa kwa kutumia lugha kwenye Mtandao. Idadi inashuka na kuwa 50% katika Waomani 48% waliojibu. Kwa hiyo, ingawa tuliwachagua wote kwa sababu wanajifunza Kiingereza, wanavyosema inaonyesha kuwa wote hawajiamini katika lugha hiyo. Lakini, matokeo haya yanaweza kuhusiana sana na kujiamini katika lugha na namna wao wanavyoiona, kama vile ustadi halisi katika Kiingereza



Matumizi ya lugha kwenye Mtandao yalipohesabiwa, iligunduliwa kwamba, kwenye sampuli kwa ujumla, Kiingereza kinatumiwa mara chache kuliko lugha za taifa katika matumizi ya Mtandao. Hata hivyo kulikuwa na tofauti kubwa katika sampuli.

NCHI	ASILIMIA YA VIPINDI ZILIZOTAJWA KWA LUGHA YA TAIFA	ASILIMIA YA VIPINDI ZILIZOTAJWA KWA KIINGEREZA
Ufaransa	86% (Kifaransa)	29%
Italia	91% (Kitaliana)	17%
Ujapani	89% (Kijapani)	15%
Macedonia	13% (Kimacedonia)	84%
Oman	100% (Kiarabu)	25%
Poland	84% (Kipoli)	49%
Tanzania	82% (Kiswahili)	90%
Indonesia	19% (Kiindonesia)	84%

Idadi hizi zinaweza kupanda mpaka juu ya 100% kwa sababu zaidi ya lugha moja ilitumiwa katika baadhi ya vipindi.

Ripoti ilionyesha kwamba Mtandao unatumiwa hasa na wahojiwa hawa kwa ajili ya kazi. Na hili ndilo lililotegemewa kwa kuchagua kundi hili kama sampuli. Baadaye data zilionyesha kuwa matumizi ya tovuti katika lugha ya Kiingereza yalikuwa chini ya kiwango kilichotegemewa. Na pale Kiingereza hakikutawala hata kama lugha ya utafiti kwenye Mtandao. Matokeo mengine yalihusu utata wa lugha ya Kiingereza inayotumiwa kwenye

tovuti, mikakati wahojiwa wanayotumia ili kukiuka matatizo ya kiufundi, jinsi mtandao wao ulivyoundwa na kuwepo kwa lugha ambazo hazitumiwi sana :

- Wahojiwa waliochaguliwa kwa ajili ya mahojiano mengine walibainisha kuwa tovuti nyingi katika lugha ya Kiingereza ambazo walizitembelea hazikuwa ‘tajiri kilugha’. Kwa mfano ni dhahiri kuwa baadhi ya matumizi ya lugha ambayo wanayoyataja yanahusiana na muziki wa *pop* au tovuti za kadi za salamu, hasa kwaa wale ambao wanakiri kutotumia sana Mtandao. Uwezekano wa lugha ya tovuti zilizo kwa Kiingereza kuwa kinaeleweka vizuri au katika namna ya maneno ya nyimbo ambazo hazieleweki vizuri zinasisitiza jambo kwamba sampuli iligawanywa katika mara mbili: wale wanaotumia Kiingereza kwa ajili ya kazi zao za Chuo kwenye Mtandao na wale ambao Kiingereza ni kama sehemu ya matumizi yao ya burudani.
- Mazungumzo yasiyo rasmi kabla ya uchunguzi yalionyesha kuwa wahojiwa ambao lugha zao hazitumii alfabeti ya kirumi mara kwa mara wanaandika lugha yao ‘kwa Kiingereza’ wakipelekea wenzao barua pepe au wakipiga soga kama hawawezi kupata kibodi na progamu za kompyuta. Kwa mfano ilionekana kuwa wanaozunguza Kiarabu wanaandika Kiarabu kwa kutumia herufi za kirumi na kujaribu kuandika mara mbili vitamkwa ‘kwa Kiingereza’. Haya yalijitokeza katika uchunguzi na katika mazungumzo ya ana kwa ana na wahojiwa. Jambo hilo halitokei tu kwenye mtandao. Waliohojiwa walisema kuwa wanatumia sana njia hiyo hiyo wanapoandika ujumbe mfupi kupitia simu zao za mkono.
- Tokeo jingine linahusiana na ufinyu wa mtandao. Kimsingi, Mtandao unaweza kutusaidia kuwasiliana na 20% za watu duniani ambao wanaweza kutumia barua pepe, lakini bila shaka, watu hawafanyi hivyo. Waliojibu walisema kuwa waliwasiliana na mitandao yao ya watu wa karibu kama familia na marafiki, na ingawa hawakuweza kuzungumza na wengine, hawakutaja kama wanazungumza nao mara kwa mara au mara nyingi. Ili kuchunguza kwa undani jambo hili, kundi moja la wahojiwa liliulizwa kama wanasoma tovuti binafsi za watafiti katika taaluma zao. Wanafanya hivyo kwa kawaida. Halafu waliulizwa kama waliwasiliana na watafiti wenyewe. Hakuna hata mmoja ambaye kawasiliana nao. Lakini hali hii inaweza ikabadilika wakiwa wakubwa na kutambuliwa wenyewe na kuwa mmjao wa washiriki katika mitando ya kimataifa.
- Tokeo la mwisho katika mapitio haya mafupi ya uchunguzi linahusika na kutoonekana sana kwa lugha ambazo hazitumiwi sana uwanjani humu katika sampuli hii. Wengi miongoni mwa kundi walitaja kuwa lugha yao ya kwanza kama lugha nyingine isiyolugha yao ya taifa, lakini hakukuwa jibu dhahiri kuhusu matumizi ya lugha hizo kwenye mtandao.

### **Mielekeo inayowezekana**

Katika watu hawa wanaozungumza lugha nyingi na ambao wana uwezo na nia ya kutumia Mtandao katika lugha zaidi ya moja, lugha za taifa zilitumiwa zaidi kuliko Kiingereza kwa ajili ya mawasiliano kwa barua pepe na soga na utafiti kwenye Mtandao.

Takwimu hizi zinatokana hasa na idadi kubwa ya waliojibu na ambao lugha yao ya taifa ni “kubwa” na “muhimu” na yenye sababu ya umaarufu inayoambatana nayo (kwa mfano, katika utafiti huu, Kifaransa, kiarabu, Kitaliana) ambao wanatumia Kiingereza mara chache tu au ambao hawakitumii hata kidogo kwenye Mtandao. Makundi haya yalijibu kuwa

hayakuhitaji sana ujuzi wa lugha mbili, labda kwa sababu wana tayari vifaa vya Mtandao katika lugha zao. Kinyume hupatikana kwa wale ambao wanazungumza lugha pale ambapo wazungumzaji wake walikuwa aidha wachache au wenye uwezo mdogo wa kiuchumi. Makundi haya yalijibu kuwa hutumia sana Kiingereza.

Hata hivyo, kulikuwa pia na kilichoonekana kwanza kama matokeo yaliyo hitilafiana kidogo kwa vile katika sampuli ambamo Kiingereza kinatumiwa mara chache (Ufaransa, Italia, Poland, Japani), kilitumia hasa kwa kukusanya habari na kwa ajili ya kazi ya Chuo. Kinyume chake, katika samples ambamo kinatumiwa sana (Macedonia, Tanzania, Indonesia), Kiingereza hakikutawala katika uwanja wowote na kilitumiwa kwa upande mmoja kuingia kwenye mtandao na kwa upande mwingine kwa kuandikia barua pepe na kuwasiliana kwa kumbi za gumzo. Lakini kwa ukweli hitilafiano hili linaweza kusuluhishwa, kwa sababu matokeo yake ni kwamba pale ambapo lugha ya Kiingereza hupanda, mtumiaji anaelekea kutumia lugha kwa ajili ya kufahamu bila ya kutumia na kwa mawasiliano ya kila siku. Hali hii ina bila shaka matokeo juu ya mazoea ya kuandika na kusoma katika miktadha hiyo, na ni jambo la 'utawala wa Kiingereza' ambao ulitajwa na kukubaliwa kama ukweli wa kijumla. Hapa sehemu ya matumizi inaweza ikachangia kwa kubadili na kutumia Kiingereza.

Mielekeo mingine iliyojitokeza ni pamoja na kuongezeka kwa kumudu mbinu za Habari na Teknolojia. Kwa muda mrefu, programu za kompyuta zilikubali tu lugha ambazo zilitumia alfabeti ya Kirumi na hazikufaidi makundi ya zile ambazo hazikutumia alfabeti hiyo, hata pia zile ambazo zilikuwa zimeendelea kiteknolojia. Siku hizi masuluhisho ya kiufundi yanaendelea kwa haraka. Lakini, hata pale ambapo hayapatikani, wale ambao ulughambili uliwa uwezo katika alfabeti ya Kirumi wanatumia ujuzi wao kwa lugha nyingine ambazo wanaweza kuziandika na kuzisoma. Matumizi yanaendelea kiasi ambacho lugha ambayo ina alfabeti mbalimbali kutumiwa na kibodi na programu za kompyuta ambazo hazizitegemei. Inaonekana kuwa ni ujuzi katika Kiingereza ambao unasaidia mikakati hiyo. Kwa njia nyingine hali hii huunga mkono hoja kuwa Kiingereza huzuia lazima matumizi ya lugha nyingine kwenye Mtandao.

### **Tofauti chache na hadhari kwa upangaji wa sera**

Wazo linalozagaa kwamba Kiingereza kinatawala kwenye Mtandao linatakiwa kuchunguzwa tena. Naam matumizi ya Kiingereza ni ma kubwa. Lakini hali hii inawahusu watu wachache sana miongoni mwa makundi na hali chache ambapo watu ambao kiingereza si lugha yao maana wanaamua kutumia kiingereza badala ya lugha yao ya taifa. Mielekeo ni kuwa kuna tofauti kwenye Mtandao badala ya uhodhi wa Kiingereza. Kiingereza kilikuwa tokeo lisilo la moja kwa moja la asili za kijiografia za teknolojia na makazi pa watumiaji wa awali. Fursa ya kutumia inavyojitokeza na kushiriki kunavyopanda katika maeneo yote ya dunia, mwelekeo kwa matumizi ya lugha mbalimbali ndivyo tu unaongezeka. Kiingereza kilikuwa pia tokeo lisilo la moja kwa moja la hali ya watumiaji wa mwanzoni ambao walikuwa wasomi wa kimataifa. Kutumia mtandao kunavyowezekana zaidi kwa watu wengi na kutoka matabaka ya juu hadi chini katika jamii, itakuwa vile vile kuhusu lugha. Wanafunzi hawa wa Chuo Kikuu wanaoweza kuonekana leo kama wasomi wa awali wanabainisha lugha za namna mbalimbali ambazo zinaambatana na kukua kwa mtandao.

Kwa ufupi, matumizi ya Kiingereza kwenye Mtandao yanaonekana kuwa yanatokea bila matatizo yoyote na matumizi ya moja kati ya lugha muhimu za taifa. Wale wanaojua lugha mbili kikiwemo Kiingereza na lugha mashuhuri ya taifa yenye wazungumzaji wengi na uchumi fulani, ambao anaweza kuunga mkono na kukuza lugha hiyo kwenye mtandao,

hawaonekani wakiacha kwa wingi lugha yao na kutumia Kiingereza kwenye mtandao. Na hapa, hata kama Kiingereza kinatumiwa mara kwa mara, inaonekana isivyoaminika kuwa hali hii itachangia matumizi ya lugha nyingine badala ya ile ya taifa. Uwelekeo huo utapungua hata baadaye maadam makundi yenye lugha kubwa yataendelea kumudu vyanzo kuwa katika lugha yao na katika alfabeti zao za kijadi. Lakini, matumizi ya lugha kwenye Mtandao huweza kuwafanya wale wenye lugha zisizo na wazungumzaji wengi kuacha lugha hizo au pale ambapo wazungumzaji wa lugha hawana uwezo wa kiuchumi kugharamia tovuti katika lugha yao. Unyumbufu na uwezo wa wale wanaotumia lugha mbili katika muktadha huchangia kutumia lugha nyingine. Matokeo hayo hayashangazi na huonyesha pale ambapo jitihada zatakiwa kutoka shirika ambayo yanahusika na kuongeza tofauti kwenye Mtandao.

Matokeo kwa lugha ambazo hazitumiwi sana na zile zilizo hatarini ni kuwa zinahitaji uchunguzi zaidi. Tofauti kwenye Mtandao inaonekana kama kuwa na maana ya tovuti nyingi kwa ajili ya lugha za kitaifa kuliko tofauti kamili. Baada ya maendeleo hayo ya kitaifa labda kutatokea wakati ambapo lugha zisizotumiwa sana na zile zilizo hatarini zikitumiwa kwa urahisi zaidi pamoja na Kiingereza lugha ya kimataifa kuliko pamoja na lugha za kitaifa haionekani hata kidogo kutokana na data hizi.